SISI NI KINA NANI?

- Kundi letu ni la watu wanaoishi sehemu ambazo ni jirani na kiwanja cha ndege cha Gatwick.
- Tuna washughulikia wale wote waliotiwa Kizuizini hapa Gatwick.
- Tumejitolea kuifanya shughuli hii kwa hiari. Hatulipwi wala hatukuajiriwa na yeyote yule; bali twajimiliki.
- Twatumia muda wetu katika kuwafajiri na kutoa misaada mbalimbali kuwasaidia wale waliozuiliwa hapa Gatwick wakiwa Tinsley House.

Tuko huru kabisa! Twajitegemea. Hatubanwi wala hatukuajiriwa na madaraka ya Uhamiaji, wala Ofisi ya wale wanaohusika na madaraka ya Ulinzi wa kambi hii.

Katika kundi letu wamo walio Wakristo Waislamu, na wengineo wa Madhehebu mbali mbali, hata wale wa Madhehebu ya Kijadi pia ni wanachama.

NI NANI TUNAOWASAIDIA?

Twamsaidia ye yote yule aliye wekwa kizuizini Gatwick. Hatuna ubaguzi wa rangi, wa Utaifa au Udini, wala Ukabila Ni ye yote yule anayetuomba msaada tunamsaidia.

SHUGHUlI TUNAZOZIFANYA

- Tumeunda mradi wa kutembelea walio tiwa kizuizini kwa kulinganisha mfungwa na mgeni wake.
- Mgeni hu leta urafiki,uhusianoi,uangalizi na misaada mnaweza kuongea juu ya maada yeyote hasa shida zina zo kusumbua
- Vifaa vya msaalani visivyo tolewa kambini na nguo za mitumba tuna ku kabidhi,

Kuwasiliana na wakili wako na kutatua hitilafu yeyote ,mgeni wako ana jukumu laku wasiliana kwa simu pia kugeuza wakili na kutoa malalamiko
.
Tunayo orodha ya mawakili stadi, hodari wanaoweza kuwakilisha maombi yako mahakamani.

MAMBO TUSIYOWEZA KUTIMIZA

Hatuna madaraka wala mamlaka ye yote ya kukutoa humu kizuizini.

Hatuwezi, wala hatuna kauli ya kuzuia usirudishwe nchi uliyotokea iwapo imeamriwa urudishwe huko. Sisi sio Wanasheria, na wala hatuchukui nafasi ya Uwakili. Hivyo basi hatuwezi kutoa ushauri wo wote wakisheria

Wageni wanaokutembelea, hawaruhusiwi kukuwekea dhamana Walakini ukitaka kuwekewa dhamana tuma maombi yako kwa: BID Ofisi iko wazi kuanzia saa nne mpaka saa sita mchana kila siku.
Simu: 0207 24703590 Fax: 0207 2473550

Shirika letu haliwezi kukupatia vifaa vya gali

TUNAVYO TEKELEZA KAZI
Unapo tuomba usaidizi tuna kuweka kwenye orodha ya kutembelewa na mgeni

Jina lako litakapo tangulia kwenye foleni ya orodha utatembelewa na mgeni baada ya siku chache

Kama una watoto,au uko chini ya miaka 18,au umekumbwa na maradhi,au huwezi kuvumilia tujulishe ili upate mgeni mara moja.

UTA FAIDIKA AJE NA KUTEMBELEWA
Mgeni ata kutembelea mara moja kila juma maadam uko kizuizini hapa Gatwick

Asi poweza kukutembelea ni sharti aku arifu ama kubadilishana na mwenzie kama ata kua likizoni.na una matatizo piga simu ofisini

Wageni wetu wana ongea kabila tofauti, lakini sio zote.ukihitaji msaada na kiingereza tuna weza mpata mgeni mnaye weza kusikizana

SIRI
Tuna heshimu sana yote utakayo tuambia na mgeni wako hakubaliwi kuyazungumza,ila wewe umpatie idhini

MALALAMIKO NA MATATIZO
Kama una maoni au mamlishi kuhusu huduma uliyo pewa nasi mjulishe mfanyi kazi yeyote ofisin. Uchunguzi uta fanywa kulingana na mpango wetu wa kutatua shida

SHERIA NA USHAURI
Unaweza kua na fursa ya kushauriwa na kusimamiwa bure Mawakili huwa ni ghali sana na si wote wema
.Kama una tatizwa na wakili wako muambie mgeni wako au vikundi vinavyo toa mashauri ya kisheria.Tunayo majina ya mawakili walio fuzu

Kama una shida au huna wakili ,kuna mshauri anaye kuja mara mbili kwa juma kutembelea kambi huyu ni hodari na hutoa huduma yake bure. Anaweza kukusimamia kesini au kukupa ushauri,uliza wafanyi kazi kambini wakupe habari zaidi

Mbele ya haja muhimu(Kama vile una hamishwa kwenu)piga simu kwa **RLC** Masaa ya jioni au mwisho wa juma - **07831 598 057**

MARADHI

Muone Daktari aliye kambini mara utakapo umwa .Kama afya yako ina kutatiza ni haki uangaliwe na kama huja ridhika na matibabu rudi umweleze

Ikiwa bado huja furahishwa ongea na wakili au mgeni wako.Na pia unaweza kulalamika kupitia utaratibu ulio pasishwa (hapo chini)

HAKI KIZUIZINI

Kuna sheria inayo kupatia haki zifwatazo maadam uko kizuizini.

Malalamishi Utaelezwa jinsi ya kufwatilizia malalamiko uchunguzi hauta dhuru kesi yako au jinsi utakavyo tendwa kambini

Mahitaji Mswaki,dawa ya meno,sabuni

Ripoti ya uhamiaji

Kama umezuiliwa, ni lazima upatiwe ripoti yako kila mwezi, ukielezwa sababu yakuendelea kuzuiliwa kwako. Kama sio hivyo basi wasiliana na ofisi ya uhamiaji hapa Tinsley na watakusaidia .

PESA Ni haki yako kupewa senti za matumizi kwa siku.Waulize wafanyi kazi jinsi utakavyo lipwa

- Ukihamishwa pengine au jelani mgeni wako hawezi kukufuata ita bidi upate mwingine piga simu
- **Harmondsworth and Colbrook =** London detainee support group. Simu 020 7226 3114/0800587 2096
- **Dover** = Kikundi cha ugenini Dover Simu : 01304 242755
- **Haslar holding Centre -** Haslar visitors Group. Simu-023 9283 9222
- **Yaris wood Detention Centre -** Yarls wood visiting Group Simu01234 708710

Tupigie wakati wowote unapotaka usaidizi

UKIWACHILIWA

Kama huna pakuenda baada ya kuwa huru na una hitaji ushauri au msaada wasiliana na **Refugees Council's one stop service;** 240-250 Ferndale Road, Brixton, London, SW9 8BB Simu: 0207 346 6700

GDWG OFFICE:

225 Three Bridges Road,
Crawley, West Sussex, RH10 1LG
Tel: (01293) 434350. Fax: (01293) 434351

FREEPHONE – 0800 389 4367

Monday - Friday 9.30am - 5.30pm
Ofisi zetu ziko wazi jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa kumi na moja unusu jioni unaweza kuwacha ujumbe wakati wowote na tuta kujibu haraka iwezekanavyo mradi umeacha jina na namba ya chumba chako

Rubani- Nic Eadie
Wasaidizi: Anna Pincus, Louise Peim

SHIRIKA LA KUSAIDIA WALIOZUILWA GATWICK

Registered Charity No. 1124328
Company limited by guarantee No.4911257
(kampuni ya mkadirio iliyo dhaminiwa kupitia No.4911257)



TAARIFA KWA ALIYE KIZUIZINI

Swahili